# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

# FAHARI YA SAME

*Maendeleo Daima*

***Toleo la Septemba 2022 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***



***Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Wakifuatilia Kikao cha Baraza la Madiwani***

# DC-MADIWANI KAGUENI MIRADI YA BARABARA NA MAJI




***Mhe:Mkuu wa Wilaya ya Same,Edward Mpogolo (kushoto) akifuatilia kikao cha Baraza la Madiwani,kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Same Anastazia Tutuba,Mwenyekiti wa Halmashauri,Mhe:Yusto Mapande,Kaimu Mwenyekiti Mhe:Mhina Mmasa na Katibu wa CCM Wilaya Hamisa Chacha.***

Mhe: Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo amewataka Madiwani wa Wilaya hiyo kuweka utaratibu wa kukagua ujenzi wa Barabara na Miradi ya maji inayotekelezwa katika Wilaya hiyo ili waweze kushauri.

Mhe:Mpogolo alitoa wito huo katika kikao cha Baraza la Madiwani ambapo alisema Serikali inatoa fedha nyingi kwa Wakala wa Barabara (TARURA) na Wakala wa huduma za maji Vijijini (RUWASA) kwaajili jya kutekeleza Miradi mbalimbali hivyo ni vyema fedha hizi zikafanyiwa ufuatiliaji.

“Nashauri muweke utaratibu wa kukagua hii Miradi ya Maji na Barabara na mpate muda wa kuijadili miradi hiyo kwenye Baraza la Madiwani,lengo ni kuongeza ufanisi na uharakishaji wa Miradi hii” alisema Mhe:Mpogolo.

Aliipongeza Halmashauri kuwaalika wawakilishi wa taasisi hizo katika Baraza la Madiwani ambapo huwasilisha taarifa zao za Utekelezaji wa Miradi lakini akasema Miradi yote ambayo taarifa zake zimekuwa zikiwasilishwa kwenye Baraza imekuwa ikifanyiwa ukaguzi kasoro Miradi ya Maji na Barabara.

“Mimi na Kamati yangu ya Ulinzi na Usalama huwa tunafanya ukaguzi wa Miradi hii na kutoa maelekezo lakini miradi hii inatekelezwa kwaajili ya kuwanufaisha wananchi na Madiwani ndio wawakilishi wa Wananchi hivyo ni vyema kwenye ratiba zenu mkaweka utaratibu wa kukagua miradi hii na kuijadili kwenye Baraza” alisema Mhe:Mpogolo.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Mhe:Yusto Mapande aliahidi kulifanyia kazi agizo hilo la Mkuu wa Wilaya ili Baraza nalo liweze kujiridhisha na ubora katika utekelezaji wa Miradi hiyo.

“Suala la ukaguzi wa hii miradi ni muhimu sana,na nikuahidi tu Mkuu wa Wilaya kwamba tutaweka utaratibu wa kukagua miradi hii”alisema Mhe:Mapande.

## MAPATO SAME YAONGEZEKA KILA MWAKA



***Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba,akikagua Vitunguu kama vimelipiwa Ushuru kabla ya kusafirishwa katika eneo la Hedaru wilayani humo.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imeendelea kufanya vizuri katika makusanyo ya mapato ya ndani ambapo kila mwaka kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato hayo.

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri ya Wilaya ya Same Ilijiwekea malengo ya kukusanya shilingi Bil.2.2 ambapo hadi kumalizika kwa mwaka wa fedha ilifanikiwa kukusanya shilingi Bil.2. sawa na asilimia 92.

Mwaka uliofuata 2021/22 Halmashauri hiyo ilikadiria kukusanya shilingi Bil.2.6 ambapo hadi mwisho wa mwaka ilifanikiwa kukusanya Bil.2.5 ambayo ni sawa na asilimia 99.2.

Akizungumzia mafanikio hayo Mkurugenzi wa Halmasahuri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba alisema ni ushirikiano mzuri uliopo miongoni mwa viongozi na wakusanyaji wa mapato.

“Katika suala la ukusanyaji mapato kwenye Halmaashauri yetu hakuna bosi,kila kiongozi na kila mtumishi anashiriki kikamilifu kulinda mapato yasipotee nah ii ndio siri ya mafanikio haya”amesema Mkurugenzi.

Amesema kwa mwaka wa fedha 2022/23 Halmashauri hiyo imejiwekea malengo ya kukusanya shilingi Bil.2.9 na jitihada zimeshaanza kuhakikisha kuwa lengo hilo linafikiwa.

Tutuba amesema timu yote ya ukusanyaji mapato ya Halmashauri tayari alishaipa maelekezo ya kutosha na anaamini lengo walilojiwekewa watalifikia”ili Halmashauri iweze kufanikiwa kuwaletea wananchi Maendeleo ni lazima tujitume katika makusanyo”alisema Tutuba.

## DED SAME AMSHUKURU RAIS KWA BIL. 6 ZA MIRADI YA MAENDELEO



***Nyumba tatu za Watumishi wa Afya Kituo cha Afya Kisiwani ambazo zimegharimu shilingi milioni 90***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu kwa kuipatia halmashauri hiyo zaidi ya shilingi bilioni 6 kwaajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/22.Tutuba alisema fedha hizo zimetumika kutekeleza miiradi mbalimbali ikiwemo ya Elimu Msingi na Sekondari, Afya,Kilimo na Mifugo.

Aliitaja baadhi ya Miradi iliyotekelezwa na fedha hizo kuwa ni Ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati na jingo la kupokea wagonjwa wa dharura katika Hospitali ya Wilaya,Ujenzi wa shule mbili mpya za sekondari (Kalemawe na Mighareni) ,ujenzi wa madarasa na Ujenzi wa Nyumba tatu za Watumishi wa Afya Kisiwani.

Mkurugenzi alisema kuwa wilaya hiyo pia imepokea milioni 640 ili kufanikisha ujenzi wa madarasa 32 kwaajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023.

Alisema fedha hizo zitamaliza tatizo la upungufu wa madarasa kwaajili ya kidato cha kwanza kwa mwaka kesho kwani Wilaya hiyo ilikuwa ina uhaba wa madarasa 32 hivyo fedha hiyo itakidhi kumaliza tatizo.

“Same tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kupatiwa fedha hizi,napenda kumuahidi Rais kwamba ujenzi huu utakamilika mapema kwani utekelezaji umeshaanza na Januari 2023 hakuna mwanafunzi atakayekosa nafasi ya kuingia kidato cha kwanza”alisema Tutuba

Alisema usimamizi wa Miradi jya Maendeleo katika Wilaya hiyo upo vizuri na kwamba ipo miradi ambayo imekamilika na mingine ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Kaimu Afisa Elimu Sekondari, Mary Sanga alisema tayari fedha za madarasa ambazo zinajumuisha na utengenezaji wa madawati zimeshapokelewa katika shule husika na utekelezaji upo katika hatua za awali.

Alizitaja shule zilizonufaika na fedha hizo kuwa ni shule za Sekondari Chauka,Lugulu,Makanya,Mkombozi,Moipo na Mvurekongei ambazo kila moja imepewa shilingi Mil.40 kwa ujenzi wa madarasa mawili,shule za Gonja na Kwambegu zimepatiwa kila moja Mil.60 kwaajili ya madarasa matatu kila moja na shule ya Ndungu imepatiwa Mil.120 kwaajili ya madarasa sita.

Shule nyingine zilizonufaika ni Irikiponi,Kibacha,Kirangare,Mabilioni Mighara,Myamba,Pareni na Vudee ambaazo kila moja imepatiwa Mil.20 za ujenzi wa darasa moja.

## VITABU VYA MIONGOZO YA ELIMU VYAZINDULIWA SAME



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe:Edward Mpogolo akionyesha vitabu vya Miongozo ya Elimu mara baada ya kuvizindua.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imezindua Vitabu vya Muongozo wa Elimu kwa ajili ya kusimamia uongozi na taaluma katika Elimu kwa upande wa shule za Msingi na Sekondari.

Akizungumza katika Uzinduzi huo Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Same Marclaud Mero alisema vitabu vilivyozinduliwa ni vitatu kikiwemo cha Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi

wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa ambacho kimeeleza kwa kina namna ya kuwapata viongozi hao.

Alitaja kitabu kingine kilichozinduliwa kuwa ni kile cha Changamoto katika Uboreshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari na nini kifanyike, ambapo alisema kitabu hiki kimeeleza changamoto zilizopo na kuweka njia ya kuzipatia ufumbuzi.

Mero alisema kitabu cha mwisho kilichozinduliwa kuwa ni cha Mikakati ya kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzi ngazi ya Elimu ya Msingi ambacho kinatoa muongozo juu ya kuboresha taaluma kwa shule za Msingi.

Akizungumza katika hafla hiyo baada ya kuzindua Vitabu hivyo,Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe:Edward Mpogolo aliwapongeza walimu kwa jitihada wanazochukua katika ufundishaji ambazo kwa pamoja zimeufanya Mkoa wa Kilimanjaro kuwa kinara katika utoaji wa elimu.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo,Anastazia Tutuba aliwataka Viongozi wote wanaosimamia elimu kuhakikisha wanasoma Miongozo hiyo na kuielewa vema na kuifuata katika kazi zao.

“Hii miongozo isomeni na muitekeleze maana katika kupima utendaji pia utekelezaji wa hii miongozo utajumuishwa katika upimaji na miongozo mingine inayoendelea kutolewa” alitahadharisha Tutuba.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 200 wakiwemo Wakuu wa shule za Msingi na Sekondari wakijumuisha wa shule za serikali na za binafsi,ilihudhuriwa pia na Maafisa Elimu Kata na wadau wengine wa elimu.

Wilaya ya Same ina shule za Msingi 202 ambapo 187 ni za serikali na 15 ni za binafsi,huku shule za Sekondari zikiwa 62 ambapo 43 ni za serikali na 19 za binafsi.



***Mhe:Mkuu wa Wilaya ya Same,Edward Mpogolo akikabidhi Vitabu vya Muongozo wa Elimu kwa Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Same,Godfrey Sebulu mara baada ya Mkuu huyo kuzindua vitabu hivyo.***

# MAKAMU MWENYEKITI WA HALMASHAURI APITA BILA KUPINGWA




***Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Mhe: Mhina Mmasa (katikaki) akiwa amerejea kwenye nafasi yake baada ya kupita bila kupingwa,kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe:Yusto Mapande na kulia ni Katibu wa CCM Wilaya,hamisa Chacha.***

Aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Mhe:Mhina Mmasa ameendelea kutetea nafasi yake hiyo baada ya kupita bila kupingwa katika uchaguzi uliofanyika kwenye kikao cha Baraza la Madiwani mwishoni mwa mwezi Agosti mwaka huu.

Katika kikao hicho Madiwani kwa kauli moja walimpitisha Mhe:Mhina Diwani wa Kata ya Bendera ambaye alikuwa mgombea pekee wa nafasi hiyo kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo.

Baada ya kupitishwa Mhe:Mhina aliwashukuru wajumbe kwa kuendelea kumuamini kuwatumikia katika nafasi hiyo ya Makamu Mwenyekiti na kuahidi kuendelea kuwa muadilifu na kushirikiana vema na wenzie ili kuleta maendeleo katika Wilaya ya Same.

“Nawashukuru sana waheshimiwa Madiwani wenzangu kwa kuendelea kuniamini katika kuitumikia nafasi hii,niwaahidi kwamba sitawaangusha,tutaendelea kupambana kuhakikisha kero za wananchi zinapungua na mapato yetu ya Halmashauri yanaongezeka”alisema Mhe:Mmasa.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mhe:Yusto Mapande alimpongeza Makamu Mwenyekiti kwa kupita bila kupingwa na kumtaka waendelee kushirikiana katika kuleta Maendeleo ya Same.

Nimefurahishwa na waheshimiwa Madiwani kuendelea kuwa na imani na Makamu wangu maana kupita bila kupingwa inamaanisha kuaminiwa sana,basi tuhakikishe hatuvunji hii imani kwa kusimama imara kuitumikia Halmashauri yetu" Alisema Mwenyekiti.

Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe: Edward Mpogolo alimpogeza Makamu Mwenyekiti kwa kuendelea kutetea nafasi yake na kumtaka kushirikiana vema na Mwenyekiti na Madiwani wenzie katika kuhakikisha kuwa Same inafikia malengo yake ya Maendeleo.

## DED-WAFANYABIASHARA CHANGAMKIENI SOKO LA KIRINJIKO




***Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba***

Wafanyabiashara Wilayani Same na maeneo ya jirani wametakiwa kuchangamkia fursa katika soko jipya la barabara kuu iendayo Dar es Salaam lijulikanalo kama soko la Kirinjiko ambalo liko mbioni kuanza kutoa huduma baada ya ujenzi kukamilika.

Mkurugunzi wa Halmashauri hiyo,Anastazia Tutuba alitoa wito huo wakati wa kikao cha Baraza la Biashara kilichofanyika mwishoni mwa mwezi Septemba ambapo aliwashauri wafanyabiashara kuwahi na kushika maeneo kwaajili ya kufanyia Biashara.

Tutuba alisema soko hilo ambalo liko takriban umbali wa kilomita 10 kutoka Same mjini kuelekea barabara iendayo Dar es Salaam linatarajia kuanza kazi rasmi muda wowote kuanzia sasa na kutakuwepo na bidhaa mbalimbali pia kutakuwa na huduma ya nyama choma na mnada wa mifugo.

"Same inalima tangawizi,vitunguu,viazi,nyanya na bidhaa zote hizi zitakuwa zinapatikana katika soko letu la Kirinjiko na hata wafugaji tunao hivyo kutakuwa na mnada wa mifugo pamoja na nyama choma zitakuwa zinapatikana,tunawashauri madereva wote wa mabasi kuingiza magari katika eneo hilo ili kuwapa fursa wasafiri kujipatia bidhaa"alifafanua Tutuba.

Akizungumzia Soko hilo Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe: Edward Mpogolo alisema Halmashauri ya Wilaya inaendelea kuweka mazingira bora ya kuwawezesha

wafanyabiashara kufanya biashara katika maeneo mbalimbali jambo ambalo pia litaongeza pato la Serikali.“Lengo letu ni kutoa fursa mbalimbali za kibiashara kwa watu wetu lakini pia kuongeza pato la serikali,katika soko letu hilo jipya la barabarani tunaweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa magari yote ya abiria yanaingia sokoni hapo”alisema Mhe:Mpogolo.

## SAME YATUMIA MIL.659 ZA MAPATO YA NDANI KUTEKELEZA MIRADI



***Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Mary Kanumba akitoa maelekezo kwa mafundi wanaojenga shule mpya ya Sekondari ya Kalemawe,kulia kwake ni Diwani wa Kata ya Kalemawe ,Mhe:Athumani Mbelwa na kushoto kwake ni Mkuu wa shule hiyo Bakari Idd.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imetumia shilingi milioni 659.3 sawa na asilimia 40 ya mapato ya ndani kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo Wilayani humo.

Afisa Mipango wa Wilaya ya Same,Mary Kanumba amesema Miradi hiyo ni utekelezaji wa agizo la Serikali kuwa kila Halmashauri inapaswa kutumia asilimia 40 ya Mapato yake ya ndani kwaajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aliitaja Miradi iliyotekelezwa na kiasi cha fedha zilizotumika kuwa ni Ukarabati wa Vibanda Kituo kikuu cha mabasi na soko la Kwasakwasa (Mil.27),Ukarabat wa mita 2,900 ya Mifereji ya Umwagiliaji (Mil.71.7),Ukamilishaji wa Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Hedaru (Mil.20).

Alisema Miradi mingine iliyotekelezwa kuwa ni pamoja na Ukamilishaji wa Bwalo la Chakula Ndungu Sekondari (Mil.30),Ukarabati Ofisi za Vijiji Mnyale na Manka (Mil.12),Uendelezaji na Utunzaji wa Miundombinu ya Halmashauri (Mil.27),Ukarabati wa Machinjio Same na Vichinjio Makanya na Ndugu(Mil.9).

Miradi mingine ni Ukamilishaji wa Ujenzi wa Nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Narema(Mil.10),Ujenzi wa darasa lenye miundombinu ya uvunaji wa maji ya Mvua Shule za Msingi Mvungwe,Jiungeni,Mfereji na Mbono(Mil.80),Matengenezo ya Madawati Shule za Msingi na Sekondari (Mil30),Mikopo kwa vikundi vya Vijana,Wanawake na Walemavu (Mil.160.5).

## WAFUGAJI WATAKIWA KUSHIRIKI UWEKAJI MIFUGO HERENI




***Ng'ombe aliyevalishwa hereni***

Halmashauri ya Wilaya ya Same inatarajia kuvalisha Hereni za utambuzi kwa mifugo 52,450 ikiwemo Ng'ombe ,Mbuzi, Kondoo na Punda hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu.

Afisa Mifugo wa Wilaya hiyo,Dk.Cainan Luponelo alisema zoezi hili lilitarajia kuanza Mwezi Septemba,2022 lakini haikuwezekana kutokana na kukosekana kwa herein hivyo zoezi hilo litaanza mapema mwezi Oktoba,2022 na litakamilika mwishoni wa mwezi huo.

Dk.Cainan amewataka wafugaji kutoa ushirikiano kwa maafisa watakaofika katika maeneo yao kwaajili ya utekelezaji wazoezi hilo ili kuiwezesha serikali kujua idadi ya mifugo iliyopo na kuweka mipango mizuri na malisho na mahitaji smengine.

"Hili zoezi lina faida nyingi ikiwemo kuiwezesha serikali kudhibiti magonjwa ya mifugo,kuwawezesha wafugaji kupata mikopo na kupata bima ya mifugo yao,lakini pia kudhibiti wizi wa mifugo"alisema.

Alisema kwa kuanzia Wilaya hiyo imeagiza hereni zenye thamani ya Tsh.5.9 mil kwaajili ya kuanza kutekeleza zoezi na zitakua zinaongezwa kulingana na uhitaji.

Alizitaja gharama za kuweka hereni kwa Ng'ombe na Punda ni Tsh.1,750 na kondoo na mbuzi Ni Tsh.1,000 gharama ambazo zitatolewa na mfugaji.

Dk.Cainan anasema mfugaji yeyote atakayekiuka zoezi hilo adhabu yake ni faini isiyopungua mil.2 au kifungo cha mwaka mmoja jela au vyote kwa pamoja.

Akizungumzia zoezi hilo mfugaji Shaaban Kiambe wa Kijiji cha Bangalala ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kinyang'a alisema wafugaji wa eneo hilo hawana pingamizi lolote na zoezi hilo.

"Tunaamini serikali inapokuja na mpango wowote kwa wananchi wake Mpango huo huwa na manufaa mengi kwa wananchi hivyo sisi wafugaji wa Bangalala tunaunga mkono zoezi hili la serikali na tutashiriki" alisema Kiambe

## 'TUNAHITAJI WAWEKEZAJI KWENYE MKONGE'



***Shamba la Mkonge lililopo Makanya Wilayani Same.***

Wilaya ya Same imetenga jumla ya Ekari 3,000 kwenye Kata ya Makanya kama eneo maalum la kimkakati kwaajili ya kuhamasisha .uwekezaji katika zao la Mkonge

Akizungumza katika Kikao Cha Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo,Mhe: Yusto Mapande alisema eneo hilo linatarajiwa kuinua uchumi wa watu wa Same na kuiongezea mapato serikali.

'Eneo hili litagawanywa katika vitalu vya Ekari 25 ambapo vitakua vitalu 120 na kila kitalu kitalipiwa Tsh. 1,000,000/- kwa mtu mwenye nia ya kuwekeza"alisema Mhe:Mapande.

Nae Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhe: Edward Mpogolo alisema Wilaya inakaribisha wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

"Watumishi na madiwani changamkieni hii fursa,na watu wa Same na nje ya Same tunawakaribisha kuja kuwekeza Same"alisema Mhe: Mpogolo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Same, Anastazia Tutuba anasema Uwekezaji huo utasaidia katika kukukuza uchumi wa Same na kuongeza mapato ya Serikali.

"Shamba hili lipo umbali wa Mita 500 tuu kutoka barabara kuu iendayo Dar es Salaam,ni sehemu inayofikika kirahisi"anabainisha Tutuba

## MILIONI 168 ZAKOPESHWA VIKUNDI

Halmashauri ya Wilaya ya Same imefanikiwa kutoa Mikopo ya shilingi milioni 168 kwa mwaka wa fedha 2021/22 ili kuviwezesha kiuchumi Vikundi vya Wanawake Vijana na watu wenye Ulemavu kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba amesema mikopo hiyo ni asilimia 10 yamapato ya halmsahauri ambayo hutengwa kwaajili ya kuviwezesha kiuchumi vikundi vya Wanawake,Vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema fedha hizo zimenufaisha jumla ya Vikundi 63 ambavyo vilikidhi sifa zote za kuweza kupatiwa fedha hizo,vikundi hivyo ni 31 vya Wanawake, 20 vya vijana na 12 vya watu wenye Ulemavu ambavyo vilitembelewa na kuonekana vimekidhi sifa.

“Tunasisitiza tu kwa Vikundi ambavyo vimepatiwa fedha hizi za Halmashauri basi viongozi wake wasimamie vema kuhakikisha kwamba zinakuwa na manufaa kwa kikundi na marejesho yanafanyika kwa wakati” alisema Mkurugenzi.

Alisema marejesho yanapowasilishwa mapema yanawezesha vikundi vingi zaidi kupata fedha na hata wale waliorejesha wanaweza kuongezewa kiasi cha fedha wanachohitaji.

Akizungumzia kuhusu urejeshaji wa mikopo ya Vikundi,Afisa Mendeleo wa Wilaya ya Same,Benedict Missani alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 marejesho yalikuwa shilingi Mil.178 ambayo ni pamoja na madeni ya miaka ya nyuma.

Amesema Ofisi yake linaendelea kufuatilia marejesho ili vikundi vingine viweze kunufaika na mikopo hiyo.

Alisema lengo la Serikali ni kuwezesha vikundi hivi ili wanachama wake waweze kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini lakini jambo kubwa wanalopaswa kufanya ni kuhakikisha fedha hizi zinarejeshwa.

“Tunaendelea kufuatilia marejesho lakini pia tunatoa elimu juu ya umuhimu wa kurejesha fedha hizi na tuna imani zitarejeshwa maana vikundi vyote vilivyopewa fedha vilitembelewa na maafisa Maendeleo wa Wilaya na kukidhi vigezo ambapo ni pamoja na kuonekana vina uwezo wa kurejesha” alisema Missani.

# SAME YAVUKA MALENGO CHANJO YA POLIO



***Watoto wakipatiwa Chanjo ya Polio katika Kata ya Hedaru***

Katika zoezi la awamu ya tatu ya chanjo ya Polio,wilaya ya Same imefanikiwa kufikia watoto 106,649 mbayo ni sawa na asilimia 195 ya lengo lililowekwa la kuchanja watoto 54,441.

Mratibu wa Chanjo Wilayani humo Happinus Pilula alisema zoezi hilo la siku nne halikua jepesi kwani Kuna baadhi ya maeneo yenye changamoto ya uwepo wa Tembo lakini walihakikisha maeneo yote yanafikiwa.

"

Wilaya yetu inajulikana Ina changamoto ya Tembo katika baadhi ya maeneo lakini katika kuhakikisha watoto wote wanafikiwa tulishirikiana na Askari wa Wanyamapori ambao waliambatana na Timu za uchanjaji katika kufikia maeneo hayo"alisema Pilula.

Alisema makadirio ya Wilaya hiyo ilikuwa kuchanja watoto 54,441 ambao ndio walioweza kuchanjwa kwa awamu ya pili ya Mwezi Mei,2022 lakini mambo yamekuwa tofauti kwani timu za uchanjaji ziliweza kufikia watoto 106,649 awamu ya tatu.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya,Alex Alexander alisema timu za uchanjaji Wilayani humo zimefanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba hakuna mtoto anayeachwa bila kupata chanjo.

"Awamu hii ya tatu ya uchanjaji tulikua na timu 123 za uchanjaji na tulikua na timu za usimamizi kwa kila Kata ambazo zilifuatilia kuhakikisha hakuna mtoto aliyeachwa,hadi tunafunga zoezi hili la siku nne tumejiridhisha kuwa tumefikia watoto wote"alisema Alexander.

Kwa Upande wake Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe: Edward Mpogolo alizipongeza timu za Chanjo kwa kufanikisha zoezi hilo vema.

Mhe: Mpogolo alisema kutokana na jitihada hizo kwa sasa Wilaya inaamini kuwa zaidi ya asilimia 98 ya watoto wapo salama dhidi ya Ugonjwa wa Kupooza ambao husababishwa na virusi vya polio.

“Nimefahamishwa kuwa kutakuwa na zoezi la chanjo ya Polio awamu ya nne mwezi Oktoba ,2022 hivyo niwaombe wasimamizi wote wa zoezi hili kusimamia kikamilifu na kuhakikisha kuwa watoto wote wanachanjwa”alisema Mhe: Mpogolo.

## SAME YAPATA WATUMISHI 308 AJIRA MPYA.

- **Ni wa Elimu na Afya**

Halmashauri ya WIlaya ya Same imepokea jumla ya Watumishi wapya 308 wakiwemo wa Afya,Elimu Msingi na Elimu Sekondari ili kuboresha utendaji katika Idara hizo za Serikali.

Akizungumza na Jarida hili Kaimu Afisa Elimu Sekondari, Mwl. Mary Sanga amesema walimu wa Sekondari waliopokelewa ni 71 ambapo 26 kati ya hao walipokelewa mwaka 2021/22 na wengine 45 wamepokelewa mwezi Julai,2022 na kwamba wamesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza uhaba wa walimu Wilayani humo.

Mwl. Sanga alisema Wilaya ya Same kwa sasa inakabiliwa na upungufu wa Walimu 162 wa Sekondari,ambapo zaidi ya nusu ya upungufu huo ni walimu wa Sayansi na wengine ni wa somo la Kiingereza hivyo ameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwapatia walimu wa Sayansi pale ajira nyingine zitakapotoka,amesema kwa sasa Wilaya hiyo ina Walimu 796 wa Sekondari.

Kwa Upande wa Elimu Msingi Jumla ya Walimu 187 walipokelewa ambapo mwaka 2021/22 walipokelewa 172 na mwezi Julai,2022 wamepokelewa 15.

Afisa Elimu Msingi,Marclaud Mero ameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza walimu zaidi kwani kwa shule za Msingi bado mahitaji ni makubwa ambapo alisema kwasasa kuna Walimu 1,136 ambapo mahitaji halisi ni 1,727 hivyo kusababisha upungufu wa Walimu 591.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya Alex Alexandra anasema Idara hiyo imepokea Wauguzi na Madaktari 50 kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambao tayari wamesharipoti kwenye vituo vyao vya kazi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba ameishukuru Serikali kwa kuipatia Wilaya hiyo watumishi kwani watasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za jamii.

“Tunamshukuru sana Mheshimiwa Raisi Samia Suluhu Hassan kwa kutupa kipaumbele katika suala la Watumishi wa Idara mbalimbali wakiwemo Walimu kwani Idara hii indo ilikuwa na upungufu mkubwa lakini kwasasa kuna nafuu” amesema Tutuba

Mkurugenzi huyo amewataka waajiriwa wapya kujituma na kusimamia majukumu yao vema kwani Serikali imewaamini na kuwapa nafasi hizo hivyo hawana budi kujituma ili kuleta tija katika nafasi wanazozitumikia.

Halmashauri ya Wilaya ya Same ina jumla ya shule za Sekondari 63,zikiwemo 43 za Serikali na 20 za Taasisi binafsi,shule za Msingi 187 za serikali na 15 za binafsi.

## WAHANGA WA TEMBO WAPEWA KIFUTA JASHO



Wilaya ya Same imetoa jumla ya Shilingi milioni 108.2 kwa wahanga waliopata athari mbalimbali zilizotokana na madhara ya Tembo na Wanyama wengine hatari.

Akizungumza Jana katika kikao cha Baraza la Madiwani Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Same, Anastazia Tutuba alisema malipo hayo ni ya madhara yaliyotokea mwaka 2021/22.

"Serikali imetoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi 646 ambao mazao yao yaliharibiwa na Tembo na mifugo yao ililiwa na fisi na kwa wahanga waliopoteza ndugu zao watatu waliouwa na Tembo"alisema Tutuba.

Alitaja Kata ambazo zimepewa kifuta jasho kuwa ni Kata za Vunta,Kalemawe, Ndungu,Maore Kisiwani,Same, Njoro, Stesheni, Kisima na Ruvu.

Alisema malipo hayo yamefanyika Baada ya serikali kufanya tathmini na kujiridhisha kuwa walengwa waliolipwa wamekidhi vigezo vilivyokua vinahitajika.

Akizungumzia kifuta jasho hicho Diwani wa Kata ya Kalemawe, Mhe:Athumani Mbelwa aliishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwalipa wananchi kifuta jasho kwani madhara yanayotokana na Tembo na fisi huwa yanatokea sana katika Kata hiyo.

"Kwakweli tunaishukuru serikali kwa kifuta jasho lakini tunaomba wahusika wa Wanyamapori watafute ufumbuzi wa kudumu wa kudhibiti Tembo katika makazi ya watu"alisema Diwani huyo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe:Yusto Mapande alisema maafisa wa Wanyamapori wamebaini kuwa Tembo hao wanaotoka hifadhi ya Mkomazi wanaingia Vijijini kufuata maji ya kunywa hivyo tayari hifadhi ya Mkomazi imeshaanza kuchimba mabwawa ndani ya hifadhi ili Tembo wasiingie vijijini kutafuta maji.

"Ni kweli Tembo ni changamoto katika Wilaya yetu lakini tatizo kubwa lilikua ni kukosekana kwa majo katika eneo la hifadhi lakini kwa Sasa vinachimbwa visima hivyo tatizo hili litakwisha"alisema Mhe: Mapande.

## 8,016 KUHITIMU ELIMU YA MSINGI SAME

Jumla ya wanafunzi 8,016 kutoka shule za Msingi 193 wanatarajia kumaliza elimu yao Msingi katika Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro.

Afisa Elimu Msingi,Wilaya, Marclaud Mero amesema kuwa maandalizi ya vijana hao yalifanyika vizuri hivyo wanategemea ufaulu mzuri.

Mero amesema wanafunzi wanaofanya mtihani mwaka huu ni wale walioandikishwa darasa la kwanza mwaka 2016 ambapo Wilaya hiyo iliandikisha watoto 8131.

"Kuna wanafunzi 200 ambao walioandikishwa katika wilaya yetu lakini sasa hawajasajiliwa kufanya mitihani kwetu na hii ni kutokana na baadhi yao kuhamia katika Wilaya nyingine kwasababu mbalimbali"alisema Mero.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Anastazia Tutuba aliwataka vijana hao kujiandaa vema kwaajili ya kufanya mitihani yao ya kuhitimu elimu ya Msingi na kuwataka wahakikishe wanafaulu kwa viwango vya juu.

"Tunategemea ufaulu mzuri na ndio maana tupo kwenye mipango ya kujenga madarasa ya kutosha kupokea kidato cha kwanza,hivyo wahakikishe wanafaulu "alisema Tutuba.

## SAME YASHIRIKI SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022 KWA MAFANIKIO



***Aliyekuwa Mjumbe wa Kamati ya Sensa Wilaya ya Same,Benedict Missani akitoa elimu kwa wananchi wa Kata ya Makanya.***

Wilaya ya Same kama ilivyokuwa kwa Wilaya nyingine nchini ilishiriki kikamilifu katika zoezi la sensa ya Watu na makazi iliyofanyika nchini kote Agosti 23,2022 ili kuweza kupata idadi kamili ya wananchi wake na hali zao za kiuchumi ili kuiwezesha serikali kupanga vema mipango ya Maendeleo kwa Wananchi wake.

Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe: Edward Mpogolo aliyekua anaongoza Timu ya Uhamasishaji alisemaWilaya ilijipanga vizuri katika hatua zote ikiwemo kuhamasisha wananchi kushiriki na kutoa taarifa sahihi zinazowahusu wakati wa kujibu dodoso.

Alisema katika zoezi hilo Wilaya ilisimamia vizuri kuhakikisha kuwa zoezi linafanikiwa kwa kuhakikisha kuwa wananchi wote waliolala kwenye Wilaya hiyo usiku wa kuamkia Agosti 23,2022 wanahesabiwa.

“Hakika tulijipanga vema kwenye zoezi la sense na tuna hakika hakuna mtu aliyeachwa bila kuhesabiwa katika Wilaya yetu”alisema Mhe:Mpogolo.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Anastazia Tutuba alisema makarani walisambazwa mapema katika vitongoji vyote 503 vya Halmashauri hiyo

ambapo kwa Vitongoji ambavyo ni vikubwa kijiografia walilazimika kuweka makarani wawili.

Alisema zoezi lilienda vizuri katika Vitongoji vyote na tunaamini takwimu zitakazotolewa zitakuwa sahihi kabisa maana hakuna Kaya iliyorukwa.

"Tofauti na makarani walikuwepo pia Watendaji Kata,watendaji Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji ambao wote hawa walishirikiana kuhakikisha kwamba zoezi linafanikiwa"Alisema Tutuba.

## MAKAZI 61,492 YASAJILIWA ZOEZI LA ANWANI ZA MAKAZI




Wilaya ya Same imesajili jumla ya Makazi 61,492 na barabara 849 katika zoezi la usajili wa Anwani za Makazi (Postcode) lililofanyika hapa nchini mwezi Machi,2022 mwaka huu.

Afisa Ardhi Wilayani Same,Angelina Sampa amesema zoezi hilo lilifanyika kwa ufanisi na kukamilika katika Kata zote 34 za Wilaya hiyo na kwamba vibao vya kuonyesha barabara ya mitaa pia vimeshawekwa.

“Zoezi hili lililenga kutambulika kwa makazi na kuwezesha kufikika kirahisi kwa makazi hayo,kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kurahisisha biashara za mtandaoni” amesema Sampa.

Alisema namba za makazi na vibao vya mitaa vinasaidia pia upatikanaji wa msaada wa haraka inapotokea dharura yoyote na pia zinasaidia kurahisisha utawala bora katika maeneo hayo.

Akizungumzia ukamilishaji wa zoezi hilo Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo alionya juu ya uharibifu wowote wa vibao vya kuonyesha mitaa.

"Kila mwananchi wa Same ana jukumu la kuhakikisha kuwa vibao vilivyowekwa vya kuonyesha mitaa na barabara vinatunza na iwapo atabainika mtu anaviharibu hatua kali zitachukuliwa dhidi yake"alionya Mkuu wa Wilaya.

Alisema zoezi la Anwani za Makazi limesaidia mitaa na barabara zote kuutambulika kirahisi hivyo hata kufikisha huduma mbalimbali inakuwa rahisi.

## WAKULIMA SAME WANUFAIKA NA MBOLEA YA RUZUKU



***Afisa Kilimo Wilaya ya Same,Omar Mhina***

Wilaya ya Same imeanza kunufaika na Mpango wa Serikali wa utoaji wa mbolea ya Ruzuku ambapo tayari wakulima zaidi ya 22,700 wameshasajiliwa katika mfumo kwaajili ya kunufaika na mpango huo wa Serikali.

Afisa Kilimo wa Wilaya hiyo,Omar Mhina alisema zoezi la Usajili lilianza mwezi Agosti mwaka huu kwa vitabu vya usajili kusambazwa kwenye Kata zote 34 za Wilaya hiyo ambapo uandikishaji ulianza ukiambatana na usajili katika mfumo.

"Muitikio wa wakulima umekuwa mzuri sana maana kuna Kata ambazo wameomba nyongeza ya vitabu vya kuandikishia wakulima na tumeshawaongeza maana lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa kila anayehitaji mbolea anapata"alisema Mhina

Alisema Ruzuku iliyotolewa na Serikali ni kubwa kwani kwa mbolea ya DAP ambayo huuzwa Tsh.131,676/- kwa mfuko wa kilo 50 kwa ruzuku mkulima ataipata kwa Tsh.70,000/- ,UREA ambayo huuzwa 124,724/- kwa ujazo huohuo mkulima anaipata kwa Tsh70,000/-

Alisema ruzuku inampa nafuu kubwa mkulima kwani anapata mbolea kwa gharama nafuu sana ukilinganisha na bei ya soko ambayo ni kubwa na hivyo kusababisha wakulima wengi kushindwa kumudu.

"Ruzuku hii haichagui wakulima wote wananufaika nayo wakiwemo wadogo,wa kati na hata wale wakubwa wenye mashamba hata yanayofikia ekari 500 na kwa kila ekari moja ruzuku inayotolewa ni mifuko miwili kwa maana ya mfuko mmoja wa kupandia na mwingine wa kukuzia"alisema Mhina.

Mzee Rajab Mleli ni Mkulima wa Kijiji Cha Msindo Wilayani humo anashukuru serikali kwa kuwajali Wakulima na kuona umuhimu wa kuweka Ruzuku katika mbolea maana ruzuku hiyo itawaongezea tija wakulima na hata mavuno yataongezeka.

Aliwataja mawakala wa mbolea ya Ruzuku waliosajiliwa wilayani Same kuwa ni Tukutane Agro Business(Same Mjini),Mariam Mkilindi (Kata ya Ndungu) na Mkazeni Agro Vet (Kata ya Hedaru).

"Bado tunaendelea kutafuta mawakala zaidi ili kuhakikisha kuwa Mkulima anapata mbolea ya ruzuku jirani kabisa na eneo lake la kilimo" alisema Mhina

## 'WANAFUNZI KULA SHULENI NI LAZIMA'




***Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya same,Yusto Mapande akizungumza katika Kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika mwishoni mwa Mwezi Agosti,2022.***

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Mhe: Yusto Mapande amesema suala la wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari kula shuleni ni suala la lazima na sio hiari tena hivyo kila Mzazi awajibike kuchangia chakula cha mtoto shuleni.

Akizungumza katika Kikao cha Baraza la Madiwani mwezi Agosti mwaka huu Mwenyekiti huyo aliwataka Madiwani na Watendaji wa Kata na Vijiji kuhakikisha kwamba wanasimamia vema upatikanaji wa chakula mashuleni.

"Tunajua wapo wazazi ambao ni wabishi na wakorofi katika kuchangia kwa hiari chakula cha watoto wao mashuleni lakini tunachosema ni kwamba hapatutatumia Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kuwatia hatiani na adhabu stahili zitachukua mkondo wake" alisema Mhe: Mapande.

Alisema kuwa sheria hiyo ya mtoto inataja mahitaji muhimu kwa ustawi wa mtoto ambayo mzazi ana wajibu wa kuyatekeleza kwa mtoto kuwa ni pamoja na kumpatia mtoto chakula,mavazi na mahali salama pa kuishi na kumlinda dhidi ya madhara yoyote.

Alisema wazazi wanapaswa kutambua kuwa lishe bora na elimu ni vitu ambavyo vinatakiwa kwenda pamoja kwani motto mwenye njaa hata akifundishwa huwa haelewi hivyo wazazi wasikwepe majukumu yao ya msingi.

Akizungumzia suala la chakula mashuleni Afisa Elimu Msingi Wilayani Same Marclaud Mero alisema shule zote za Msingi Wilayani humo kuna utaratibu wa wazazi kuchangia chakula cha watoto wao mashuleni na utaratibu huu unasimamiwa na Kamati za shule na viongozi wa serikali waliopo .

"Wilaya ina shule za Msingi 187 za serikali na zote zimejiwekea utaratibu wa kuchangia chakula ili wanafunzi wale shuleni na wanakula japo wapo wazazi wanagoma kuchangia na hawa ndio watakaochukuliwa hatua kwa mujibu wa makubaliano ya Kijiji husika"alisema Mero.



JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

S.L.P 138,SAME

***Septemba 2022 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***